



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
WIZARA YA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO  
BARAZA LA MICHEZO LA TAIFA



6 Machi, 2025

TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

Baraza la Michezo la Taifa (BMT) limetoa kibali kwa bondia **Charles Leonard Tondo** chini ya **Chite Ukae Sports Promotion**, atakayesafiri tarehe 8 machi, 2025 kwenda nchini Uingereza kushiriki pambano la ubingwa wa 'Common Wealth Youth Super bantam weight' linalotarajiwa kufanyika tarehe 14 Machi, 2025.

Tondo anatarajia kupanda ulingoni dhidi ya bondia muingereza **Lennon Mulligan** katika uzito wa kilo 55.3 katika pamabano la raundi 10 katika ukumbi wa Crowne Plaza Hotel, Congress Road, Glasgow, G38QT, Uingereza

Charles Leonard Tondo mpaka sasa anatamba kwa jumla ya mapambano ishirini na tano (25), ameshinda mapambano kumi na sita (16), amepoteza mapambano sita (6), ametoka sare mapambano matatu (3).

Baraza linamtakia kila la heri katika pambano hilo na mapambano mengine ili kuendelea kujiweka katika rekodi nzuri pamoja na kuendelea kuipeperusha vyema bendera ya Tanzania kimataifa

Imetolewa Na:

Najaha Bakari

Afisa Uhusiano na Mawasiliano.



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
WIZARA YA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO  
BARAZA LA MICHEZO LA TAIFA



6 Machi, 2025

**TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI**

Baraza la Michezo la Taifa (BMT) limetoa kibali kwa bondia **Abubakari Ally Lubanja** chini ya **Three T Sports Promotion**, aliyesafiri tarehe 4 machi, 2025 kwenda nchini Uingereza kushiriki pambano lisilo la ubingwa la ngumi za kulipwa linalotarajiwa kufanyika tarehe 7 Machi, 2025.

Lubanja anatarajia kupanda ulingoni dhidi ya bondia muingereza **Thomas Welland** katika uzito wa kilo 57 katika pamabano la raundi 6 katika ukumbi wa Brighton Centre, Brighton, Sussex

Bondia Abubakari Ally Lubanja mpaka sasa anatamba kwa jumla ya mapambano nane (8), ameshinda mapambano matano (5), amepoteza pambano moja (1), ametoka sare mapambano mawili (2).

Baraza linamtaenia kila la heri katika pambano hilo na mapambano mengine ili kuendelea kuijiweka katika rekodi nzuri pamoja na kuendelea kuipeperusha vyema bendera ya Tanzania kimataifa

Imetolewa Na:

Najaha Bakari

Afisa Uhusiano na Mawasiliano.



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
WIZARA YA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO  
BARAZA LA MICHEZO LA TAIFA



6 Machi, 2025

TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

Baraza la Michezo la Taifa (BMT) limetoa kibali kwa bondia **Abdul Zugo** chini ya **Alson Sports Promotion**, aliyesafiri tarehe 4 machi, 2025 kwenda nchini Ghana kushiriki pambano kuwania ubingwa wa 'WBO Africa Super Light' linalotarajiwa kufanyika tarehe 6 Machi, 2025.

Zugo anatarajia kupanda ulingoni dhidi ya bondia Mghana **Faisal Abubakari** katika uzito wa 140 Lbs katika pamabano la raundi 12 katika ukumbi wa Bukom Boxing Arena, Accra, Ghana

Bondia Abdul mpaka sasa anatamba kwa jumla ya mapambano kumi na nne (14), ameshinda mapambano kumi na mbili (12), hajapoteza pambano, ametoka sare mapambano mawili (2).

Baraza linamtaenia kila la heri katika pambano hilo na mapambano mengine ili kuendelea kuijiweka katika rekodi nzuri pamoja na kuendelea kuipeperusha vyema bendera ya Tanzania kimataifa

Imetolewa Na:

Najaha Bakari

Afisa Uhusiano na Mawasiliano.